# 12. Uhifadhi wa pembejeo za kilimo

## Mada ya 12b

# Ujenzi unaofaa wa ghala la pembejeo za kilimo

CropLife AFRICA MIDDLE EAST

IFDC

# JARIDA LA UHAKIKA

## 12. Uhifadhi wa pembejeo za kilimo

## Mada ya 12b: Ujenzi unaofaa wa ghala la pembejeo za kilimo

Aina ya ghala la pembejeo za kilimo (linalouza bidhaa za kemikali kama viuawadudu na mbolea) inafanya kuwa na **ghala lililojengwa vizuri** kuwa jambo la muhimu sana. Hoja zifuatazo ni muhimu kuzingatiwa unapojenga ghala la pembejeo za kilimo:

1. Vyumba vilivyotenganishwa.
2. Nyenzo zinazotumiwa katika ujenzi.
3. Kufunga/kuzuia chochote kinachomwagika.
4. Upitishaji hewa na udhibiti wa joto.
5. Mwangaza
6. Mlango wa dharura .
7. Hali ya usalama .

**1. Vyumba vilivyotenganishwa**

Ghala la pembejeo za kilimo lafaa liwe na vyumba vingi vilivyotenganishwa:

- Chumba cha kuhifadhi kemikali: Chumba chafaa kitengwe kwa kuhifadhi pembejeo za kilimo na eneo fulani litengwe kwa upimaji wa uzito lililo na vifaa vinavyofaa.
- Chumba cha kuhifadhi vifaa: Cha kuhifadhi vinyunyizio aina ya shanta (knapsack), vifaa visivyopitisha maji, glavu, vipumulio, na kadhalika.
- Chumba cha kubadilisha: Eneo la bwelasuti (ovaroli) na buti, na eneo lingine litengwe la nguo za kawaida na liwe na njia ya moja kwa moja ya kuelekea kwa bafu la manyunyu.
- Bafu la manyunyu na basini: Eneo hili liwe na sabuni.
- Eneo la kusafisha ukitumia mtiririko wa maji: Ubamba wa saruji na kuta ili kuzuia maji kuelekezwa kando na upepo, vizuizi vya mtiririko, sehemu ya kutiririsha maji machafu kwenye shimo, maji masafi yanayotiririka, na mipira ya kutumia kumwaga maji.
- Eneo la kulowa/sampu: La kusanya maji chafu. Sehemu hii inafaa ilainishwe na udongo wa mfinyazi (centimita 10) na chokaa (centimita 5).

**2. Nyenzo zinazotumiwa katika ujenzi**

Kuhifadhi pembejeo za kilimo kunahusishwa na hatari mbili kuu: hatari ya moto kutokea na hatari ya kemikali kumwagika. Kwa hivyo, ni muhimu kutumia nyenzo za

ujenzi ambazo hazichomeki kwa urahisi na hazifyonzi kemikali zilizomwagika. Nyenzo bora kutumia ni kama:


- Kuta za saruji zilizoimarishwa kwa kutumia chuma.
- Sakafu zizisopenya au kupitisha maji. Sehemu ya juu ya sakafu iwe laini na nyororo ili kurahisishwa usafishaji wa kemikali zilizomwagika.
- Eneo la paa lisilovuja maji, lenye nguvu na la kudumu sana.

**3. Kufunga/kuzuia chochote kinachomwagika**

Sakafu zafaa zijengwe kwa njia ambayo, maji na kemikali zinazomwagika hazitiririki nje ya chumba au nje ya jengo. Inapendekezwa sana kwamba ghala la pembejeo za kilimo liwe na eneo la chini ya ardhi la kushika maji/kemikali itakapomwagika kwa kiasi kikubwa; hasa pahali viuawadudu vya majimaji vinapohifadhiwa.

**4. Upitishaji hewa na udhibiti wa joto**

Maeneo yote ya ghala la pembejeo za kilimo yafaa yawe na tundu za kupitisha hewa ili kukubalia mvuke sumu na uvundo/harufu kutoroka kutoka kwa jengo. Ghala hili lazima liwe na tundu za kupitisha hewa kwenye kuta zote. Inapendekezwa paa liwe na tundu za kupitisha hewa ili kukubali mvuke sumu kutoroka kutoka kwa jengo. Paa lazima liwe na kihami ili kupunguza joto kutoka nje. Katika vyumba, madirisha yafaa yawe juu sana ili kuingiza mwangaza na pia kuzuia mianga ya jua dhidi ya kuangukia moja kwa moja kawa bidhaa zilizohifadhiwa; Madirisha ya juu pia hufanya ndani mwa ghala kuwa baridi.




**5. Mwangaza**

Maghala ya pembejeo lazima yawe na mwangaza wa kutosha. Ghala lafaa liwe na madirisha ya kawaida ili kuwawezesha wafanyikazi kuona vizuri wanapofanya kazi, hata kama mwangaza wa nguvu za umeme haupo. Wateja wanafaa wawe na uwezo wa kusoma kibandiko cha maelezo bila shida yoyote. Katika maeneo yasio na nguvu za umeme mianga ya jua lazima itosheleze kupitia madirisha au milangoni.


**6. Mlango wa dharura**

Maghala yote ya pembejeo za kilimo lazima yawe na zaidi ya mlango mmoja ulio rahisi kufungua. Kama utafungwa na kufuli, lazima funguo ziwekwe karibu na mlango.

**7. Hali ya usalama**

Pembejeo za kilimo zinaweza kusababisha uharibifu mkubwa kwa binadamu na mazingira kama hazitashughulikiwa vizuri. Ni muhimu kuzingatia hali ya usalama unapojenga ghala. Hatua zifuatazo za usalama zinapendekezwa:

- Milango ya kuingilia lazima itengenezwe kwa mbao nzito au chuma na ifungulie ikielekea nje ya jengo/chumba.
- Lango au vizuizi vya ziada lazima viwekwe katika maeneo yalio na hatari kubwa
- Chuma za kuimarisha dhidi ya wizi lazima ziwekwe katika madirisha yote.
- Milango yote lazima iwe inayoweza kufungwa.
- Eneo la ghala lafaa lizingirwe na ua na kutumia lango lililo sahihi.
- Lazima kuwe na ishara za onyo/ilani za kutosha katika kila sehemu. Mifano ni kama: hatari; ghala la pembejeo za kilimo; hakuna kuingia bila idhini; tumia mavazi ya kujikinga; usile wala kunywa; hatari ya moto; usivute sigara.
- Ghala liwe na kinga dhidi ya wanyama waharibifu. Tundu za kupitisha hewa zifunikwe na wavu ya waya



# MWONGOZO

## 12. Uhifadhi wa pembejeo za kilimo

## <u>Mada ya 12b:</u> Ujenzi unaofaa wa ghala la pembejeo za kilimo

### Vifaa vinavyohitajika:

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi
- ☑ Karatasi kubwa

### Muda unaohitajika:

Dakiki 45

### Maandalizi:

- ☑ Makaratasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa: *Ujenzi unaofaa wa ghala la pembejeo za kilimo*
- ☑ Karatasi kubwa lililo na mchoro wa ghala la pembejeo za kilimo (tazama mfano ulioko katika makaratasi ya vitendo)
- ☑ Kundi la kadi za rangi zilizo na maandishi:
  - *Vyumba vilivyotenganishwa*
  - *Nyenzo za ujenzi*
  - *Kufungia/kuzuia chochote kinachomwagika*
  - *Upitishaji hewa*
  - *Udhibiti wa joto*
  - *Mwangaza*
  - *Milango ya dharura*
  - *Hali ya usalama*

# Mwanzo

**U**sikivu: Uliza washiriki kama washawahi kujenga ghala la pembejeo za kilimo. Wale ambao hawajawahi watapata fursa ya kujenga.

**K**ichwa: Waambie kichwa ukiwaonyesha karatasi lililo na kichwa: *Ujenzi unaofaa wa ghala la pembejeo za kilimo.*

**K**usadikika: Elezea uzoefu wako katika ujenzi wa ghala la pembejeo za kilimo.

**M**alengo: Kuelezea ujenzi unaofaa wa ghala la pembejeo za kilimo.

**M**anufaa: Kujua jinsi ya kujenga ghala la pembejeo za kilimo kutakusaidia kuboresha ghala lako.

**M**welekeo: Katika kipindi hiki, tutaangazia ujenzi unaofaa wa ghala la pembejeo za kilimo na sio pahali pa kujenga au upangaji wa bidhaa zilizo ndani.

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waambie washiriki kwamba sasa watajenga ghala lao vile walivyoahidiwa. Wagawanye katika vikundi vine. Patia kila kikundi karatasi kubwa na kundi la kalamu za kutilia alama.
2. Waambie kwamba ni lazima tuzingatie vitu fulani kabla ya kujenga ghala la pembejeo za kilimo. Kila kikundi kitachora **ghala la pembejeo za kilimo** na waonyeshe kwenye mchoro sehemu zilizo muhimu. Mchoro uwe wa kawaida; wanaweza tu kutumia nyenzo za kujenga zinazopatikana kwa urahisi katika makazi yao. Kubali muda wa kutosha kwa zoezi hili. Tembelea vikundi ukiviongoza.
3. Jadili **matokeo**. Kila kikundi kibandike mchoro wao katika ukuta. Tafuta usawa huku ukijadili hoja zifuatazo: vyumba vilivyotenganishwa, nyenzo za ujenzi, kufungia au kuzuia kemikali zilizomwagika, upitishaji hewa, udhibiti wa joto, mwangaza, milango ya dharura, na hali ya usalama. Kila unapojadili mojawapo ya hoja, bandika kadi ya rangi ukutani na utaje vile kila kikundi kiliionyesha katika mchoro. Kwa mfano, kikundi hiki kilichora chumba kimoja tu. Unafikiri hili ni wazo nzuri? Kwa nini chumba kimoja hakitoshi? Hakikisha umejadili hoja zote zilizotajwa katika karatasi za vitendo.
4. Onyesha washiriki mchoro ulioutengeneza wa ghala la pembejeo za kilimo.

# Malizia

**M**uhtasari: Tumia mchoro wako kutoa muhtasari. Taja vyumba vilivyotenganishwa, nyenzo za ujenzi, kufungia au kuzuia kemikali zilizomwagika, upitishaji hewa, udhibiti wa joto, mwangaza, milango ya dharura, na hali ya usalama.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Uliza kwa nini upitishaji hewa ni muhimu katika ghala la pembejeo za kilimo na kwa nini tuzingatie hali ya usalama. Waulize mahitaji ya chini sana ya kuta na sakafu.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki tumejifunza kuhusu ujenzi unaofaa wa ghala la pembejeo za kilimo. Katika kipindi kitakachofuata, tutajifunza kuhusu kupanga bidhaa katika ghala la pembejeo za kilimo.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.